# CHUO CHA UFUNDI ARUSHA

A: MASHARTI MAALUM YA MKATABA

| | | |
|---|---|---|
| 1 | MWAJIRI | Mkuu wa Chuo<br>Chuo cha Ufundi Arusha<br>S. L. P...296......... |
| 2 | JINA NA ANWANI YA FUNDI (*Mwajiriwa*) | Jina:..GOODLUCK..LEMAO<br>Anwani:..549..........<br>Simu:...0784.-.312597 |
| 3 | ENEO LA UJENZI | *CHUO CHA UFUNDI ARUSHA* |
| 4 | MAELEZO YA KAZI KWA UFUPI | *KAZI YA UMALIZIAJI WA JENGO LA MAABARA, MADARASA NA OFISI* |
| 5 | GHARAMA YA UFUNDI (+ *Skills Development Levy)* | *(Gharama za kazi zimebainishwa katika jedwali 4.1)* |
| 6 | MUDA WA MKATABA<br>(Tangu Kusainiwa kwa Mkataba): | Tarehe ya Kusaini ..18:11:2021<br>Muda:..180...*(Taja idadi siku)*<br>Tarehe ya Kuanza Kazi ...18:11:2021<br>Tarehe ya Kumaliza Kazi .19.:05:.2022<br>*(N.B:Tarehe ya kuanza na kumaliza kazi ni baada ya fedha kuingia )* |
| 7 | MASHARTI YA MALIPO: | • Hakuna Malipo ya Awali<br>• Malipo yatafanyika baada ya kazi husika kukamilika na kukaguliwa. |

## 4.1 Jeduali la mchanganuo wa kazi

MUANISHO WA GHARAMA ZA KAZI YA UMALIZIAJI WA JENGO LA MAABARA, MADARASA NA OFISI

JINA LA FUNDI ......GOODLUCK LEMAO.........

| GHARAMA ZA UFUNDI ZA UMALIZIAJI WA JENGO LA MAABARA, MADARASA NA OFISI | | |
|---|---|---|
| NA | MAELEZO | GHARAMA (TSHS) |
| 1.0 | **KAZI ZA UASHI** | |
| 1.1 | Kujenga tofali za kuta zote zilizobaki katika ground floor, 1st floor, 2nd floor na 3rd floor kama mchoro unavyoelekeza | 8,000,000.00 |
| 1.2 | Kuandaa eneo la ndani nje ya jengo, kuweka timazi, na kupiga ripu (1:4) kuta, nguzo, ngazi (staircase), ngazi za kawaida, corrido na eneo lote la chumba cha lift. | 42,000,000.00 |
| 1.3 | Kuweka rough floor katika ground floor, 1st floor, 2nd floor na 3rt floor, ngazi za kawaida, rampu, ngazi (staircase) | 12,000,000.00 |
| 1.4 | Kuweka marumaru katika ground floor, 1st floor, 2nd floor na 3rd floor Pamoja na ngazi za kawaida, staircase na corrido zote kama mchoro unavyoelekeza. Kazi hii ni Pamoja na kupaka grout maeneo yote | 44,300,000.00 |
| 1.5 | Kuweka maru maru ukutani (full height) mwa mabafuni yote (ground, 1st, 2nd na 3rd floor) Pamoja na kupaka grout maeneo yote | 12,000,000.00 |
| | **JUMLA KAZI YA RIPU, SAKAFU NA MARU MARU** | **118,300,000.00** |
| | | |
| 2.0 | **KAZI YA MADIRISHA NA MILANGO** | |
| 2.1 | Kufitisha fremu zote za madirisha ya grill kama mchoro unavyoelekeza | 7,000,000.00 |
| 2.2 | Kufitisha fremu zote za milango kama mchoro unavyoelekeza | 10,500,000.00 |
| 2.3 | Kufitisha milango yote (MKONGO) nje na ndani ya jengo kama mchoro unavyoelekeza | 6,000,000.00 |
| 2.4 | Kufitisha milango ya chooni (flash door) kama mchoro unavyoelekeza | 2,000,000.00 |
| | **JUMLA YA KAZI ZA MADIRISHA NA MILANGO** | **25,500,000.00** |
| | | |
| 3.0 | **KUPAUWA (STEEL TRUSS) NA CEILING** | |
| 3.1 | Kukata, kutengeneza na kufirisha "steel truss" juu ya wall plate na kupaka redoxide na rangi | 11,000,000.00 |
| 3.2 | Kufitisha bati (IT-5) juu ya kenchi la chuma kama mchoro unavyoelekeza | 6,300,000.00 |
| 3.3 | Kurekebisha downpipe (ground, 1st, 2nd, 3rd) zilizopo na kuweka downpipe mpya na kumalizia kazi ya gata katika 3rd floor | 10,000,000.00 |
| 3.4 | Kuweka blundering (40x40cm), kufitisha gypsum bodi na mikanda yake, kazi hii na Pamoja na kufunga fibre tape na kuskimu | 12,000,000.00 |
| | **JUMLA YA KAZI YA KUPAUWA** | **39,300,000.00** |
| | | |
| 4.0 | **KAZI YA PLUMBING** | |
| 4.1 | Kuvunja sakafu, kufitisha na kuweka mfumo wa maji safi na maji taka | 40,000,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| | (bomba za ukubwa tofauti) katika ground floor, 1st ,2nd na 3rd floor | |
| 4.2 | Kufitisha vifaa mbalimbali vya plumbing (urinals, basin, WC Asian, Western, sink, gull-tap, toilet paper dish, soap dish, flush tank, gate valves n.k ) na fittings mbalimbali katika ground floor, 1st ,2nd na 3rd floor | 5,000,000.00 |
| 4.3 | Kuchimba na kujenga chemba na gulls mbalimbali, kulaza bomba za kusafirishia maji taka na kuunga katika mfumo wa kusafirisha maji taka uliopo mwishoni mwa fensi ya Chuo | 6,000,000.00 |
| | **JUMLA YA KAZI YA PLUMBING** | **51,000,000.00** |
| | | |
| **5.0** | **KAZI YA UMEME NA NETWORK** | |
| 5.1 | Kuchimba kuta na kuweka conduits za umeme na network katika maeneo yaliyosahaulika katika ground floor, 1st ,2nd na 3rd floor | 6,000,000.00 |
| 5.2 | Kufanya wiring ya umeme katika ground floor, 1st ,2nd na 3rd floor | 12,000,000.00 |
| 5.3 | Kufanya wiring ya network katika ground floor, 1st ,2nd na 3rd floor | 12,000,000.00 |
| 5.4 | Kufunga vifaa mbalimbali vya umeme (switch socket, main switch, bulb n.k) katika ground floor, 1st ,2nd, 3rd floor , kuchimba na kufitisha earth rod katika ground floor | 5,000,000.00 |
| 5.5 | Kufunga vifaa mbalimbali vya network katika ground floor, 1st ,2nd, 3rd floor . kuchimba mkonge wa kuunga network kutoka kwenye server mpaka kwenye jingo husika | 5,000,000.00 |
| | **JUMLA KUU KAZI YA UMEME NA NETWORK** | **40,000,000.00** |
| | | |
| **6.0** | **KAZI YA RANGI** | |
| 6.1 | Kuandaa ukuta,kufanya skiming na kupaka koti ya prima na koti tatu za rangi ya silk katika kuta za ndani pamoja na vyumba vyote (ground,1st,2nd na 3rd) | 19,000,000.00 |
| 6.2 | Kuandaa ukuta,kufanya skiming na kupaka koti ya prima na koti tatu za rangi weathergurd katika kuta za nje kuzunguka jengo zima (ground,1st,2nd na 3rd) | 6,000,000.00 |
| 6.3 | Kuandaa dari na mikanda,kufanya skiming na kupaka koti ya prima (ground,1st,2nd na 3rd) | 8,500,000.00 |
| 6.4 | Kupiga rangi madirisha yote, Grill za chuma na kupiga polish katika milango yote(ground,1st,2nd na 3rd) | 2,281,737.51 |
| | **JUMLA YA KAZI ZA RANGI** | **35,781,737.51** |
| | **JUMLA KUU** | **309,581,737.51** |
| | **RETENTION-5%** | **15,494,086.8755** |
| | **WITHHOLDING TAX - 5%** | **15,494,086.8755** |
| | **JUMLA KUU KWA GHARAMA ZA UMALIZIAJI WA JENGO LA MAABARA, MADARASA NA OFISI** | **278,593,563.759** |

**B: MASHARTI YA JUMLA MKATABA**

1. Fundi atafanya kazi kwa mujibu wa mchanganuo wa kazi aliopewa kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi, kwa mujibu wa maelekezo ya Msimamizi wa mradi 'clerk of work'.

2. Mwajiri atatoa vifaa vyote vya ujenzi kwa wakati kulingana na maelekezo ya Msimamizi wa mradi. Zaidi ya hayo mwajiri atatoa maji na umeme

3. Mwajiri atatoa vitendea kazi vyote kama toroli, karai, ndoo, ngazi na kifaa kingine kitachohitajika wakati huo kulingana na uhitaji wa kazi na pia mwajiri atatoa vifaa vya usalama kazini mfano koti, kofia ngumu na buti ambapo fundi Mkuu atakuwa na jukumu la kuvilinda, kuvitunza na kuhakikisha vinatumika kazini mara baada ya kukabidhiwa.

4. Fundi atafanya kazi kwa awamu mbili (2) kwa mujibu wa mchanganuo wa kazi *(kama inavyooneshwa katika kijeduari hapa chini 4.1)* na mwongozo wa Msimamizi wa Mradi, kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi.

5. Fundi asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kumsimamisha kazi na kulipa hasara zote zilitokana na uzembe au makusudi.

6. Fundi ataloa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na atahusika moja kwa moja kwenye ujenzi kwa kutumia vibarua wake na kuwaunganisha mafundi wote aliowaajiri kuhakikisha kazi inafanywa kulingana na taratibu za kiujenzi.

7. Fundi kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na asiajiri kabisa mtu asiyekuwa na utaalumu au ujuzi wa kutosha.

8. Fundi atahusika na vitendo *(kama wizi, uharibifu wa mali za chuo)* vyote vinavyofanywa na mafundi wake na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake.

9. Fundi kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la ujenzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.

10. Kiasi cha asilimia 5% ya kiasi cha mkataba kitashikiliwa na Mwajiri kwa muda wa Miezi Sita baada ya kazi kukamilika *(Retention Money)* na kulipwa mara baada ya ukaguzi wa mwisho kufanyika.

11. Ucheleweshaji wa Kazi:

    - Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi, fundi atapewa adhabu ya kulipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshwaji huo.

12. Ucheleweshaji wa Vifaa na Malipo:

    - Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwajiri *(kutokana na fedha au vifaa)*, Fundi ataongezewa muda wa kumalizia kaz

13. Uvunjwaji wa Mkataba:

- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya Chuo.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Fundi wake hatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi yake, ikiwemo kufuata michoro au maelekezo ya Msimamizi wa mradi.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi Mkuu hatakuwepo eneo la kazi kwa wiki moja (1) na kutoudhuria vikao viwili (2) vya ukaguzi wa mradi 'site meeting' bila taarifa rasmi.

14. Maelekezo ya kazi yatatolewa na Msimamizi Mkuu wa kazi (Clerk of works) na mwajiriwa (Fundi) ataomba malipo fedha kwa kazi aliyoifanya kwa mkuu wa Chuo kupitia Msimamizi wa kazi na atalipwa endapo ukubwa wa kazi aliyofanya itakaguliwa.

15. Malipo ya Fundi Mkuu yatafanyika kwa njia ya 'eletronics' MUSE kupitia akaunti yake husika.

**MWAJIRI:**

**Saini:** [signature]

**Jina :** Arnold J. Mushi

**Cheo:** Mkiti

**Tarehe:** 18/11/2021

**FUNDI:**

**Saini:** [signature]

**Jina:** GOODLUCK LEMAO

**Cheo:** FUNDI MKUU

**Tarehe:** 18.11.2021

**SHAHIDI WA MWAJIRI**

**Saini:** [signature]

**Jina:** SADI ISSA

**Cheo:** C.O.W

**Tarehe:** 18/11/2021

**SHAHIDI WA FUNDI**

**Saini:** [signature]

**Jina:** OMARY ABDALLAH ZOO.

**Cheo:** Fundi Msaidizi

**Tarehe:** 18/11/2021